IBE International Bureau for Epilepsy

ILAE International League Against Epilepsy

# IBE and ILAE Joint Statement
# Chanjo za COVID-19 na wagonjwa wa Kifafa

Chanjo dhidi ya COVID-19 zinaendelea kuidhinishwa na kupatikana kwa wanaohitaji.

Kwa sasa hakuna ushahidi unaoashiria kama, kuwa na ugonjwa wa kifafa kunachangia kuibuka kwa athari hasi kutokana na chanjo ya COVID-19. Kwa watu wenye kifafa, hatari ya kuambukizwa COVID-19 na kuzuka kwa madhara zaidi ya kiafya, inapita athari hasi za chanjo ya COVID-19.

Lakini, kama ilivyo na chanjo zingine, homa inaweza kuzuka baada ya kupokea chanjo ya COVID-19. Hii inaweza kuongeza matukio ya kuanguka kwa baadhi ya wagonjwa wa kifafa. Lakini, wakitumia madawa ya homa, kama vile Paracetamol /acetaminophen kwa muda wa masaa 48 baada ya chanjo aukipindi chote wanachougua homa, hatari hii inapungua.

Kabla ya kupokea chanjo ya COVID-19, hakikisha umemjulisha anayetoa huduma ya chanjo kuwa wewe ni mgonjwa wa kifafa. Kadhalika mpe taarifa zingine muhimu kuhusu afya yako kama vile;

- mizio haswa mzio dhidi ya kiungo chochote katika chanjo
- mizio yoyote iliyochochewa na chanjo za awali (historia)
- kama una homa yoyote sasa au uliwahi kuugua hivi karibuni
- aina zote za madawa unayotumia (kama kunayo), haswa madawa yanayodhoofisha uwezo wa mwili kujiami dhidi ya magonjwa; au dawa za kuzuia damu kushikamana
- kama u mja mzito (una mimba), unanyonyesha au unanuia kutunga mimba

Kama ilivyo ada na chanjo zingine, usipokee chanjo ya COVID-19 kama una mizio na kiungo chake cho-chote. Usipokee dosi ya pili kama ulipata mizio kutokana na dosi ya kwanza

Ni muhimu kwa wale ambao tayari wamechanjwa dhidi ya COVID-19, kuendelea kuvaa barakoa, kunawa mikono na kukaa umbali wa mita moja na nusu. Chanzo zinazotumika sasa zinapunguza hatari ya kupata ugonjwa wa COVID-19 kwa takriban asilimia 90 (90%), ikitegemea aina hasa uliyopewa. Walakin, watu waliopokea chanjo ya COVID-19 wanaweza bado kusambaza virusi vya COVID-19 bila kutambua kuwa wanavibeba.

IBE-epilepsy.org ILAE.org

